MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA TAREHE 18/02/2021 KATIKA UKUMBI MKUBWA WA MANISPAA

KU/SMC/KU/42/2020 – WALIOHUDHURIA:

A. WAHESHIMIWA MADIWANI

1.	Mhe. Jastin Malisawa	-	Mstahiki Meya – Mwenyekiti
2.	Mhe. Istus Kapufi	-	Naibu Meya
3.	Mhe. Dimela Kafwa	-	Diwani viti maalum
4.	Mhe. Juma Mnanka	-	Diwani Kata ya Msua
5.	Mhe. Adorfina Konongo	-	Diwani Kata ya Lwiche
6.	Mhe. Frank Lupimo	-	Diwani Kata ya Milanzi
7.	Mhe. Francis Manyika	-	Diwani Kata ya Majengo
8.	Mhe. Mary Kipalasha	-	Diwani Kata ya Malangali
9.	Mhe. Hadija Maufi	-	Diwani Viti Maalum
10.	Mhe. Edwin Misasi	-	Diwani Kata ya Katandala
11.	Mhe. Roswita Chekwe	-	Diwani Viti Maalum
12.	Mhe. Janeth Sinyangwe	-	Diwani Viti Maalum
13.	Mhe. Colnel Kafumu	-	Diwani Kata ya Sumbawanga
14.	Mhe. Anthony Kayombo	-	Diwani Kata ya Chanji
15.	Mhe. Gabriel Kimamala	-	Diwani Kata ya Izia
16.	Mhe. Charles Chakupewa	-	Diwani Kata Ya momoka
17.	Mhe. Andrea Cheka	-	Diwani Kata ya Kizwite
18.	Mhe. Juma Dawood Nzegere	-	Diwani Kata Mazwi
19.	Mhe. Agustino Ngoani	-	Diwani Kata yaPito
20.	Mhe. Syriacus Pangani	-	Diwani Kata ya kasensne
21.	Mhe. Cadius Mtullo	-	Diwani Kata ya Ntendo
22.	Mhe. Leticia Kipeta	-	Diwani Viti Maalum
23.	Mhe. Sangu Maarifa	-	Diwani Kata Mollo0
24.	Mhe. Anna Mwamba	-	Diwani Viti Maalum
25.	Mhe. Lameck Pondamali	-	Diwani Kata ya Mafulala

B. WATAALAM

1.	Ndg. Jacob J. Mtalitinya	-	Mkurugenzi Manispaa – Katibu
2.	Ndg. Maxmillian Babile	-	Mratibu wa UKIMWI
3.	Ndg. Tulimbujo Mwasandube	-	Afisa Utumishi
4.	Ndg. Scolastica Mwakatobe	-	Kaimu Afisa Elimu Msingi
5.	Ndg. Marykiada Mwanji	-	Kaimu DACC
6.	Ndg. Happy Kyasi	-	Afisa Ustawi wa Jamii

C. SEKRETARIETI

1.	Ndg. Khadija Dalasia	- Katibu wa Vikao

KU/SMC/KU/23/2020 – KUFUNGUA KIKAO:

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao, Mwenyekiti alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema. Aliwaomba wajumbe waweze kujitambulisha kwani kikao hiki ni kikao cha kwanza tangu uchaguzi Mkuu ufanyike hivyo wengi ni wageni. Aliwaomba wajumbe waweze kuchangia kwa umakini ili kikao kiweze kuwa kifupi. Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 5:52 Asubuhi.

KU/SMC/KU/43/2020 – KUTHIBITISHA DONDOO:
Ziliwasilishwa dondoo za kikao cha tarehe 17.02.2021 wajumbe kwa kauli moja walizipokea na kuzithibitisha.

KU/SMC/KU/44/2020 – KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 04.06.2020
Muhtasari ulisomwa na ulifanyiwa masahihisho Uk 1 kisha Katibu na Mwenyekiti waliuwekea saini.

KU/SMC/KU/45/2020 – TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 04.06.2020
Iliwasilishwa taarifa ya utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha tarehe 04.06.2020.
Taarifa ilipokelewa.

Hoja
Mhe. Mstahiki Meya alipenda kufahamu iwapo Msimamizi wa eneo la Maziko anatoa na vibali vya Maziko?

Jibu
Mganga Mkuu aliwaambia wajumbe kuwa Afisa Afya huyu anaotoa vibali kwa ajili ya Mpangilio wa eneo hilo na sio nani anazikwa katika eneo hilo.

Ushauri
Eneo hili la Maziko liboreshwe kwa kuwekewa Miundo Mbinu katika eneo hilo la Maziko kama vile kuweka Taa na Ujenzi wa Uzio.
Majukumu ya Msimamizi ya Maziko yawekwe bayana na Wakuu wa Taasisi wajulishwe ili kusiwe na Muingiliano wa Majukumu.

AZIMIO
Ifikapo Tarehe 25.02.2021 Choo cha Stendi kiwe kimekalika na kianze kutumika ili kuongeza Mapato.

KU/SMC/KU/46/2019 – TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA MWEZI DESEMBA 2020

Mweka Hazina aliwasilisha taarifa ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha Mwezi Desemba 2020 na wajumbe walichangia kama ifutavyo:

Hoja
Mhe. Istus Kapufi alipenda kufahamu iwapo Halmashauri inapa ushuru wowote wa Machinjio kutoka Machinjio ya SAAF

Jibu
Afisa Mifugo na Uvuvi aliwaambia wajumbe kuwa Halmashauri haipati chochote kutokana na Uchinjaji kutoka katika Kiwanda cha SAAF kwani Mkoa walizuia.

Hoja
Mstahiki Mweya alipenda kufahamu ni kwanini Ushuru wa Soko uko Chini kwani umekusanywa kwa asilimia 0.01.

AZIMIO
Ifikapo Mwezi April 2021 Machinjio ikamilike na kuanza kufanya Kazi .

Hoja
Mhe. Hadija Maufi alipenda kufahamu ni kwanini Baadhi ya Kata Kama 8 hazijawekewa Kasma ya Ukusanyaji wa Vibali vya ujenzi.

Jibu
Mweka Hazina aliwaambia wajumbe kuwa Kata hizi zimekwisha endelezwa na mapato yao yanaingia Katika Mapato Mengineyo.

Ushauri
Watendaji wa Kata waainishe vyanzo vya Mapato kwa uhalisia kwani mapato yapo.

Hoja
Mhe. Edwin Misasi alipenda kufahamu ni kiasi gani kinakusanywa kutokana na Minara kwani Katika Kata minara iko mingi ila kiasi kinachokusanywa ni kidogo sana.

Jibu

Mweka hazina aliwaambia wajumbe kuwa Minara Mingi iko kwa watu binafsi na Michache inayokusanywa na Halmashauri.

Hoja
Mhe. Lupimo alipenda kufahamu ni kwanini Kata ya Milanzi hakuna Kasma ya Ukusanyaji wa Madini.

Jibu
Mweka Hazina aliwaambia wajumbe kuwa Chanzo cha Madini kinakusanywa na Makao Makuu na zinasomwa kwenye kifungu cha makao Makuu.

Azimo
Idara ya Fedha Ifuatilie Chanzo cha Mapato cha Pombe za Kienyeji katika Kata za Nje kwani kuna upotevu wa mapato

KU/SMC/FU/2021 TAARIFA YA UTEKELEZAJI KAZI KWA KIPINDI CHA OKTOBA – DESEMBA 2020

A. TAARIFA YA MANUNUZI
Afisa Manunuzi aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi kwa kipindi cha Oktoba-Desemba 2020.

Hoja
Mhe. Manyika alipenda kufahamu soko la Mandela ni lini litaanza kufanya kazi na kiasi cha tsh Mil 300 alizo ahidi Rais zimeshaletwa.
Jibu
Mkurugenzi aliwaambia wajumbe kuwa ujenzi unaoendelea hapo ni kwa nguvu ya Mapato ya Ndani na wannachi walikuwa wamepewa muda hadi tarehe 28.02,2021 wawe wamekamilisha ila wameomba kuongezewa muda.
Hivyo Soko hilo litafunguliwa ifikapo tarehe 30.06.2021

Taarifa ilipokelewa.

B. TAARIFA YA MKGAUZI WA NDANI
Mkaguzi wa ndani aliwasilisha taarifa ya Mkaguzi wa ndani kwa kipindi cha Oktoba – Desemba

Hoja
Wajumbe walipenda kupata ufafanuzi kuhusu fedha za uchaguzi n kwani kuna hoja nyingi ambazo mwisho wa siku inaweza kusababisha hati chafu

Jibu
Mkurugenzi aliwaambia wajjumbe kuwa Fedha ya Uchaguzi ilikuja na imetumika sawa na Bajeti, na hakuna deni na majibu yameshapatikana.

Hoja
Wajumbe walipenda kufahamu kwanini kuna deni katika fedha za EP4R kwani fedha hizi zinakuja na miongozo.

Jibu
Mkurugenzi aliwaambia wajumbe kuwa Fedha hizi zilikopwa mwaka 2018 kwa ajili ya ukamilishaji wa madarasa na pindi Halmashauri itakapokamilisha itarejesha fedha hizo.

Taarifa ilipokelewa

C: TAARIFA YA KITENGO CHA TEHAMA

Afisa Tehama aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi kwa kipindi cha Oktoba- Desemba 2020.

Taarifa Ilipokelewa

D: TAARIFA YA KITENGO CHA SHERIA

Mwanasheria wa Manispaa aliwasilisha taarifa ya ya utekelezaji kazi kwa kipindi Mwezi Oktoba – Desemba 2020.

Ushauri

Halamsuari ikae na Kuona kama inaweza kukubaliana na watu wanaotudai nje ya Mahakama ili tuweze kupunguza madai katika Halmashauri zetu.

F: TAARIFA YA KITENGO CHA UCHAGUZI

Afisa uchaguzi aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi toka kitengo cha Ustawi wa Jamii kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Desemba 2020

Wajumbe walipongeza menenjimenti kwa namna ambavyo wameweza kusimamia uchaguzi vizuri.
Taarifa ilipokelewa.

G: TAARIFA YA MIRADI YA MAENDELEO

Afisa Mipango Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi kwa kipindi cha Oktoba – Desemba 2020.

Taarifa ilipokelewa.

KU/SMC/FU/2021 TAARIFA MBALIMBALI

A. MPANGO MKAKATI WA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA KWA SHULE ZA SEKONDARI JANUARI 2021- NOVEMBA 2021

Afisa Mipango Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa ya Mpando Mkakati wa Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa kwa shule za Sekondari Januari 2021- Novemba 2021.

Hoja

Mhe. Mwenyekitialipenda kufahamu iwapo Halmashauri itagharamia ujenzi wote wa vyumba hivyo vya Madarasa kuanzia Msingi hadi kupaua?

Jibu

Mkurugenzi aliwaambia wajumbe kuwa Halmashauri itatoa fedha kwa kata ambayo itafikisha maboma katika usawa wa linta na ndipo watapewa Milioni Nane kwa kila Boma.

Taarifa Ilipokelewa

B. TAARIFA YA UJENZI WA SHULE YA SEKONDARI UTENGULE

Afisa Mipango Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa ya Ujenzi wa Shule ya Sekondari utengule.

Taarifa Ilipokelewa.

C: TAARIFA YA KUTHIBITISHA WAJUMBE WA BODI YA MANUNUZI

Afisa Manunuzi aliwasilisha Mapendekezo ya Wajumbe wapya wa Bodi ya Zabuni ambao wanachukua nafasi ya Wajumbe waliomaliza Muda wao na wengine Kustaafu.

Wajumbe wapya hao ni

1.	Frank Mateni	-	Afisa Maendeleo ya Jamii	-	Mwenyekiti
2.	Andrew Zumba	-	Afisa Uchaguzi	-	Mjumbe
3.	Thadeo Maganga	-	Afisa Misitu	-	Mjumbe

Kamati iliridhia Maombi hayo.

D: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA AWAMU YA PILI KISI CHA BILIONI MOJA KWA AJILI YA UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA .

Afisa manunuzi aliwasilisha taarifa ya Mapokezi ya fedha awamu ya pili Kiasi cha Tsh Bilioni Moja kwa ajili ya Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

Hoja
Mhe. Ewin Misasi alipenda kufahamu ni kwanini fedha za awali zilizopokelewa hazikuweza kutumika zote hadi zikapelekea kurudishwa TAMISEMI.

Jibu
Mkurugenzi aliwaambia wajumbe kuwa Fedha hizo zilirudishwa kwa sababu Halmashauri ilishindwa kutumia Fedja hizo kwa wakati na ni kwasababu fedha hizo ziliingia kwa kuchelewa.

Hoja
Mhe. Mstahiki Meya alipenda kujua Gharama za Kuvunja Msingi wa jengo la OPD ni nani anayezibeba kwani ni hasara

Jibu
Mkurugenzi aliwaambia wajumbe kuwa hasara za ubomoaji huo zinabebwa na Halmashauri kwani mwanzoni jengo hilo lilikuwa linajengwa na Magereza na ikaonekana Msingi alioujenga ni mrefu sana ambao ungeleta madhara hapo baadae.

I: TAARIFA YA VYUMBA VYA BIASHARA KATIKA STENDI YA KATUMBA AZIMIO

Afisa Manunuzi aliwasilisha taarifa ya Vyumba vya Biashara katika Stendi ya Katumba Azimio na kusema kuwa wanatarijia kufungua Stendi kwa Muda kulingana na Ushauri wa Mtaalamu Mshauri. Kwamba Mfumo wa Maji na mfumo wa Umeme vikishakamilika Stendi hiyo inaweza kufunguliwa kwa muda kwa kutumia jengo la Chini.

Hoja
Mhe. Mwenyekiti alipenda kujua ni kwanini gharama za Mradi zimeongezeka ?

Jibu
Afisa Manunuzi aliwaambia wajumbe kuwa Gharama za mradi zilizbadilika baada ya vikao vya kisheria kuridhia mabadiliko ya Mchoro kwa kuongeza jengo hilo kuwa jengo la ghorofa moja.
Taarifa Ilipokelewa
F: TAARIFA YA UONDOSHWAJI WA MAGARI MACHAKAVU
Afisa manunuzi aliwasilisha taarifa ya Uuzwaji wa Magari Machakavu ambayo ni Nissani na Gari ya Chanjo
Hoja

Mhe Kiparasha alipenda kufahamu iwapo magari hayo yanayotakiwa kuondoshwa yapo hapa na yanaondoshwa kwa kiasi gani?
Jibu
Mkurugenzi aliwaambia wajumbe kuwa

KU/SMC/KU/47/2020 – KUFUNGA KIKAO:
Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao aliwwashukuru wajumbe kwa michango yao mizuri ambayo ina nia ya kuiletea maendeleo Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe ambao wao ndio kikao chao cha kwanza kushiriki wameshiriki kikamilifu kwa kuwa wawazi na kuchangia mengi yenye tija. Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 1.40 Usikuc-p;; 3 .

Umesambazwa na ……. Saini ……. Tarehe ……

UMETHIBITISHWA / HAUKUTHIBITISHWA

……	…….
Jacob J. Mtalitinya	Mhe. Istus Kapufi
Mkurugenzi Manispaa	**Naibu Meya**
KATIBU	**MWENYEKITI**